**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MARA

**DODOMA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MARA
S.L.P 193, MUSOMA Email: marasec123@gmail.com
Tovuti: www.marasecondaryschool.blogspot.Com

**NAMBA ZA SIMU**
**Mkuu wa shule: 0762-177-350**
**Makam wa Shule: 0683-484-252 0624-573-995**
**Mtaaluma: 0625 91 21 25 0752 39 32 32**

**JINA LA MZAZI/MLEZI WA: ……………………………………………………………………….**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MARA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA- MKOA WA MARA MWAKA................**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na masomo ya Kidato cha **TANO** tahasusi ya ____________________katika shule ya sekondari **MARA** ambapo atapata Elimu na hatimaye kulitumikia Taifa. **Kama Mzazi/Mlezi unapaswa kumuasa mwanao azingatie masomo pamoja na taratibu zote za shule na kumpa mahitaji yote ya shule ili aweze kulifikia lengo hili la Kitaifa. Aidha, aelewe kuwa ni miongoni mwa watanzania wachache waliopata nafasi hii adhimu na anapaswa kuitumia vyema.**

Shule ya Sekondari Mara ipo umbali wa **Kilometa 9** Kusini mwa mji wa Musoma. Usafiri wa pikipiki/basi kutoka stendi kuu ya manispaa ya Musoma unapatikana katika kituo cha mabasi Bweri kwa Nauli ya **Tsh 500** kwa basi (Daladala), pikipiki ni **Tsh 3,000/-** na **5,000/-**kwa bajaji.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **................** Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **..............** Muda wa kuripoti ni kuanzia saa **2:00 asubuhi** hadi saa **11:00 Jioni** siku za kazi Tu. Mwanafunzi anatakiwa kuwa ameripoti shuleni si zaidi ya **wiki mbili (siku 14)** tangu tarehe ya muhula wa kwanza kuanza. Mara mwanafunzi afikapo shuleni aripoti Ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule kwa ajili ya mapokezi na Usajili.

Pia mwanafunzi ajapo shuleni ni muhimu aje na vitu vifuatavyo;

i). Mahitaji yote yaliyoelekezwa katika fomu hii
ii). Fomu iliyojazwa na Daktari katika hospitali ya **SERIKALI** kuhusu Afya ya Mwanafunzi (**Medical Examination Form**).
iii). Fomu iliyojazwa ya maelezo binafsi ya mwanafunzi (**Personal Particularas Form**).

iv). Fomu ya kukubali masharti ya shule. Wewe na mwanao muisome kwa kina pamoja na sheria za shule mkizikubali, msaini fomu hizo na ziwasilishwe shuleni hapa wakati wa kuripoti.

v). Aje na Ream ya karatasi (**Double A**) Zinatakiwa **4** kwa mwaka au **2** kwa muhula.

vi). Fomu ya usajili wa mzazi/mlezi/ndugu wa karibu wa mwanafunzi.

vii). **BIMA YA AFYA** au **50,400** kwa ajili ya Kutengenezewa Bima ya Afya kama Hana (**NI LAZIMA**)

**ZINGATIA**: **HATUPOKEI MWANAFUNZI SIKU NA SAA AMBAZO SIYO ZA KAZI.**

**……………………………………..**

**MKUU WA SHULE**

**1- Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**1.1- Sare za Shule**

i). Sare ya shule ni suruali nyeusi (02) kwa Wavulana. Suruali iwe na turn-up na upana wa 18cm.

ii). Mashati meupe mawili (02) ya mikono mirefu.

iii). Soksi nyeusi ndefu jozi mbili (02)

iv). Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.

v). Tai yenye nembo ya shule-inapatikana shuleni kwa Tsh 6,000 kwa atakayehitaji

vi). Sweta ya rangi ya ugoro (yenye michirizi mirefu mitatu myeupe mikononi na ubavuni) yenye mshono wa V shingoni,yenye nembo na maandishi ya shule-inapatikana shuleni kwa Tsh 27,000 kwa atakayehitaji

vii). Viatu vyeusi vya shule vya kufunga na kama na vyenye visigino vifupi.

viii). Suruali mbili (02) za kushindia zenye rangi ya DARK BLUE **kitambaa namba 01**

ix). Viatu vya michezo-Raba za michezo

x). Jezi ya Taifa Stars (Angalia picha pg Namba 8)

xi). Track suit rangi ya **Dark Blue** yenye michirizi meupe pembeni, nembo na maandishi ya shule inapatikana shuleni kwa Tsh 35,000. Vazi hili litavaliwa kila ijumaa siku za masomo kwa atakayehitaji

xii). T-shirt nzito yenye kola, nembo na maandishi ya shule inapatikana shuleni kwa Tsh 25,000 (kwa T-shirt moja). Vazi hili litavaliwa siku ya jumatano ya kila wiki kwa atakayehitaji

**1.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i). Madaftari ya Quire 3 kuanzia 6

ii). Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa iii). Aje na nakala yamatokeo (Result slip) ya kidato cha nne

iii). Spring FILE 1

iv). Kalamu za wino wa blue na nyeusi za kutosha

v). Penseli za kuchorea **HB NO 2**

vi). **Aje na solar taa kwa dharura ya mwanga pale umeme unapokatika**

vii). Ream nne (04) kwa mwaka au ream mbili (02) kwa muhula (Kwa kila mmoja)

viii). Dissecting Kit kwa wanafunzi watakaosoma somo la Biology,inapatikana shuleni kwa Tsh 25,000 kwa atakayehitaji

ix). Koti la maabara (Lab Coat) nyeupe kwa wanafunzi wa sayansizinapatikana shuleni kwa Tsh 35,000 kwa atakayehotaji

**x). Oxford Advanced Dictionary Tsh 45,000/- inapatikana kwenye duka la shule. (NI LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI) kwa atakayehitaji**

xi). Scientific calculator kwa wanafunzi watakao soma masomo ya Economics,Geography,Physics,Chemistry,Advance Mathematics na Basic applied Mathematic zinapatikana shuleni kwa Tsh 45,000 kwa atakayehitaji

xii). Godoro jipya lenye vipimo vya 2½ X 6 X 6-yanapatikana kwenye duka la shule.

xiii). Mashuka ya Light Blue jozi mbili-yanapatikana kwenye duka la shule

xiv). Blanket 1 na foronya ya godoro 1

xv). Chandarua cha rangi ya blue 1 (**NI LAZIMA**) -zinapatikana kwenye duka la shule

xvi). Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe)-vinapatikana kwenye duka la shule.

xvii). Ndoo moja (01) ndogo ya ujazo wa lita kumi (10) na mfuniko wake.zinapatikana kwenye duka la shule

xviii). Chombo cha maji ya kunywa (container) ujazo wa Lita mbili (02) vinapatikana kwenye duka la shule.

xix). Viatu vya wazi (**OPEN SHOES**) ila visiwe viatu vya Crooks au yeboyebo-vinapatikana kwenye duka la shule

xx). Ndala kwa ajili ya kuogea-zinapatikana kwenye duka la shule

### 1.2 Vifaa vya kazi au usafi

| WOTE WAJE NA: | MAHITAJI YA KILA TAHASUSI | |
|---|---|---|
| -Soft broom 1 na Fyekeo 1 | **PCB** | Ream ya A3 1 |
| -Hard Broom 1 | **PCM** | Aro (Dawa) 1 na Jemba na Mpini wake 1 |
| -Mopa (Squeezer) 1 | **PGM** | Ream ya A3 1 |
| -Fagio wa chelewa 1 | **HKL** | Koleo moja (01) |
| - | **HGK** | Shoka na mpini wake moja (01) |
| -Dawa ya chooni aina ya **Dexy** all-purpose cleaner **lita 05** - Sabuni nyingine haitopokelewa. | **HGE** | Ream ya A3 1 |
| | **HGL** | Aro (Dawa) 1 na Jemba na Mpini wake 1 |
| | **CBG** | Mkasi wa kukatia Mauwa au fensi |
| | **EGM** | Panga moja (01) na Jemba na Mpini wake 1 |
| Mahitaji yote haya yanapatikana kwenye duka la shule | | |

**NB**: Matibabu; Mwanafunzi aje na Bima ya Afya ya NHIF, AAR au 50,400 kwa ajili ya kujiunga na bima ya afya ya NHIF (**NI LAZIMA**)

### 1.3 Michango mbalimbali

#### a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi | AKAUNTI YA MALIPO |
|---|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000 | |
| 2 | Tahadhari | 5,000 | |
| 3 | Nembo | 5,000 | NMB - 30301200288 |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000 | JINA: **MARA SECONDARY SCHOOL** |
| | **Jumla** | **80,000** | |

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 2.1- Sheria na Kanuni za Shule

**2.1.1-** Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

**2.1.2-** Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

**2.1.3-** Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);

**2.1.4-** Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

**2.1.5-** Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

**2.1.6-** Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

**2.1.7-** Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

**2.1.8-** Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

**2.1.9-** Kutunza mali za shule;

**2.1.10-**Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

**2.1.11-**Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

**Kwa wanafunzi wanaotokea mbali anaruhusiwa kuja na simu na wakati wa kuripoti anatakiwa kuikabidhi kwa makamu mkuu wa shule na si mwalimu mwingine.Simu hiyo atakabidhiwa tena baada ya kufungashule na si vinginevyo.Ikiwa mwanafunzi atakamatwa na simu atalipa fedha ya uharibifu wa miundombinu ya shule Tsh 250,000/-**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule ambapo mzazi/mlezi atatakiwa kuja kumchukua mtoto endapo changamoto itajitokeza. (Msiba au Ugonjwa**).

**2.2- Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

**2.2.1-** Wizi;
**2.2.2-** Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 14 bila taarifa;
**2.2.3-** Kugoma na kuhamasisha mgomo;
**2.2.4-** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
**2.2.5-** Kumpiga , kupigana na mwanafunzi mwenzake, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
**2.2.6-** Kuwa na nywele ndefu zisizokubalika shuleni.
**2.2.7-** Kufuga ndevu;
**2.2.8-** Ulevi au unywaji wa pombe
**2.2.9-** Uvutaji wa sigara; (matumizi ya dawa za kulevya)
**2.2.10-**Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
**2.2.11-**Kusababisha mimba;
**2.2.12-**Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
**2.2.13-**Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
**2.2.14-**Kumiliki, kukutwa au kutumia **SIMU YA MKONONI** (Nje au Ndani ya mazingira ya shule)
**2.2.15-**Kudharau Bendera ya Taifa;
**2.2.16-**Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; nk
**2.2.17-**Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
**2.2.18-**Kuvuka na kukutwa NJE ya mipaka ya shule WAKATI WOWOTE bila RUHUSA**.**

## 3- Viambatisho na Fomu Muhimu

| | |
|---|---|
| i). | Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali; |
| ii). | Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai; |
| iii). | Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na |
| iv). | Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza |

kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MARA**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0762-177-350**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0684 484 252/0624 573 995**
- **Mwandamizi Taaluma 0625 91 21 25/ 0752 39 32 32**
- **Mwandamizi Malezi 0712 555 575**



**4.0: Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:**

i. Fomu ya hospitali (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara mwanafunzi atakaporipoti shuleni.

ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, makosa ya jinai.

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

iv. Barua/fomu ya kukuita shuleni.

**5.0: Hitimisho muhimu**

Tafadhali soma kwa umakini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu

1. Hatupokei fedha taslimu shuleni. Hivyo malipo yote yapitie **BENKI** isipokuwa malipo ya vifaa vinavyoweza kupatikana shuleni.

2. Mwanao haruhusiwi kuja shuleni na simu ya kiganjani, pasi ya umeme, redio, heater, computer na TV. AKIPATIKANA NA VIFAA HIVI, ADHABU NI KUONDOLEWA SHULENI PAMOJA NA KULIPA FIDIA YA UHARIBIFU WA MIUNDOMBINU YA SHULE KIASI KISICHOPUNGUA TSH. 250,000/=

3. Haturuhusu mwanafunzi kutembelewa shuleni na watu wasio fahamika.

4. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi bwaloni mara kengele ya chakula inapogonga akiwa na vyombo vya chakula.

5. Shule haina utaratibu wa kutoa chakula maalum (special diet) kwa wale wenye matatizo ya kiafya ya kutokula baadhi ya vyakula.

6. Mwanafunzi atumiwe nauli mapema kabla ya kufunga shule ili utaratibu wa usafiri uweze kuandaliwa mapema.

7. Ratiba ya shule huanza saa 11:30 Alfajiri kwa mchakamchaka, kufanya usafi binafsi na usafi wa mazingira ya bwenini.

8. Mwanfunzi ataruhusiwa kusali katika dhehebu lake shuleni kulingana na utaratibu uliowekwa na shule.

9. Mawasiliano ya mwanfunzi na mzazi/mlezi yapitie katika uongozi wa shule. HATURUHUSU MWANAFUNZI KUPIGA SIMU SHULENI, BALI ATATUMIA UTARATIBU WA MAWASILIANO ULIOWEKWA NA SHULE.

Hakikisha mwanao anakuja na mahitaji yote muhimu na anaripoti kwa wakati akiwa na;

- Barua/Fomu hii ya kujiunga shuleni.
- Bank pay slip original ya malipo ya kulipia benki.
- Nakala ya Result Slip inayoonyesha matokeo ya kidato cha IV.
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa kama anacho.
- Fedha ya kulipia mahitaji yanayopatikana shuleni kama ilivyoelekezwa kwenye fomu.
- Vifaa/mahitaji yote muhimu kwa matumizi binafsi/shule.
- Fomu ya hospitali na maelezo binafsi zijazwe kwa usahihi.

**SCHOOL MOTTO: "ELIMU NA KAZI"**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MARA.**

**<u>FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA TARATIBU ZA SHULE</u>**

**SEHEMU YA I: IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE**

Mimi………………………………………………………………. Nimezisoma **sheria ,kanuni na taratibu za shule** na kuzielewa vizuri bila ya shaka yoyote. Ninaahidi kuzitii na kutozivunja katika kipindi changu chote cha kusoma kwangu katika shule ya MARA sekondari. Vilevile, nitajitahidi kusoma kwa bidi na kushiriki shughuli zote za nje kulingana na ratiba ya shule. Endapo nitakwenda kinyume na kiapo cha ahadi yangu, basi uongozi wa shule unichukulie hatua za kinidhamu ikiwa ni Pamoja na **kupewa adhabu kali/kusimamishwa masomo na hata kufukuzwa shule.**

**Dini………………………………Dhehebu……………………………Tarehe ya kuzaliwa……………...**

**Michezo uipendayo/Hobbies…………………………………………………………………………...**

**Kazi ya mzazi/mlezi……………………………………………mahali……………………………………….**

**Wilaya……………………………………….Mkoa…………………………Simu…………………………**

**Jina la mwanafunzi……………………………………………..Sahihi……………………Tarehe……….**

**SEHEMU YA II: IJAZWE NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

Mimi……………………………………………………………………ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ..........................................................................................kidato cha tano mwaka 2025;

Ninakiri kuwa nimeyasoma maelekezo ya kujiunga na shule ya sekondari MARA na kuyaelewa vizuri. **<u>Ninaahidi</u>** kushirikiana na uongozi wa shule katika kuhakikisha mwanangu anazingatia taratibu zote za shule wakati wa kipindi chote cha masomo yake. Pia, **<u>nitampatia</u>** mahitaji yake yote muhimu ya shule ikiwa ni Pamoja na malipo, mahitaji binafsi na kufuatilia mwenendo wake kitaaluma na nidhamu na **<u>niko tayari</u>** kupokea maamuzi yoyote yatakayotolewa na uongozi wa shule endapo mwanangu atavunja taratibu, kanuni na sheria za shule.
Mwisho, endapo nitashindwa kutimiza jukumu langu la kumlipia mwanangu ad ana michango halali ya shule kwa wakati, niko tayari kuwajibishwa ikiwa ni Pamoja na kufikishwa katika vyombo vya kisheria kwani kufanya hivyo ni kuzorotesha maendeleo ya mwanangu na mipango ya shule kwa ujumla.

**Jina la mzazi/mlezi………………………………………………Sahihi…………………Tarehe…….**

**…..................SEHEMU YA III: UHUSIANO WA MWANAFUNZI NA NDUGU/JAMAA WENGINE.**

Tafadhali jaza majina, namba za sim una kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ndugu/jamaa wa mwanafunzi kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano na uongozo wa shule.

| | **JINA LA NDUGU** | **UHUSIANO** | **NA. SIMU** | **ANAKOISHI** | **KAZI** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |

**ASANTE KWA USHIRIKIANO**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MARA
S.L.P 193, MUSOMA Email: marasec123@gmail.com
Tovuti: www.marasecondaryschool.blogspot.Com

## FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. JINA ........................................................ DINI ..................................................
2. TAREHE YA KUZALIWA.................................3. KIJIJI ULIMOZALIWA.............................
4. TARAFA ULIMOZALIWA ............................5. WILAYA ULIMOZALIWA ..........................
6. MKOA ULIMOZALIWA .................................. KAMA UNAKAA MJINI ..........................
7. TAJA MJI:.....................................MTAA.........................BARABARA.................................
8. JINA LA BABA.......................................9. KAZI YA BABA...........................................
10. ANWANI YA BABA..............................................................................................................
11. JINA LA MAMA .................................... 12. KAZI YA MAMA..........................................
13. ANWANI YA MAMA ............................................................................................................
14. JINA LA ATAKAYEHUSIKA NA MWANAFUNZI KIPINDI CHOTE CHA MASOMO:
    JINA:.................................................. ANWANI:........................................................
    SIMU:.................................................. EMAIL: ..........................................................
15. 

| SHULE ULIZOSOMA | MADARASA | MADARAKA ULIYOSHIKA |
|---|---|---|
| ...................................... | ........................ | ............................................ |
| ...................................... | ........................ | ............................................ |

16. JE, BABA YU HAI? ..................................... (NDIYO/HAPANA)
17. JE, MAMA YU HAI? ..................................... (NDIYO/HAPANA)
18. JE, UNAKAA NA MLEZI ................................ (NDIYO/HAPANA)
19. ANWANI YA MLEZI ..............................................................................
20. KAZI YA MLEZI ..................................................................................
21. ELEZA MATATIZO YA NYUMBANI, YA MAGONJWA, N.K. YANAYOKUKABILI
...........................................................................................................................
22. UNAFIKIRI MATATIZO HAYO YATATATULIWA VIPI? ...........................................
...........................................................................................................................
23. ELEZA MIPANGO YAKO YA MAISHA YA BAADAYE
...........................................................................................................................
24. MKO WANGAPI KATIKA FAMILIA? (A) WA KIUME ..............................................
    (B) WA KIKE ............................... (C) WEWE NI WA NGAPI ................................
    (D) NDUGU WANGAPI WAMEAJIRIWA ? ..................................................................
25. KAZI AMBAZO UNGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO
...........................................................................................................................
26 KAZI AMBAZO USINGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO
...........................................................................................................................
26. JINA ............................................ SAHIHI................... TAREHE.................................

**VITABU MUHIMU KWA MWANAFUNZI**

**PHYSICS**

1. Principle of physics for class XII & XI by S.Chand (2011)
2. Physics form five By TIENB. Angalau ununue kimoja

**MATHEMATICS**

1. Scientific calculators
2. Basic and Applied mathematics by TIE
3. Mathematics for class Xi & XII by DASS,H.K & VERMA,R.(2000)
4. Advance Mathematics form five by TIENB: Angalau ununue kimoja

**BIOLOGY**

1. Dissecting kit- Muhimu
2. Laboratory Coat
3. Biological Science by Taylor,etal (1997)- Muhimu4. S.Chand's Biology for class XI & XII byP.SVerma & B.P Pandey (2005).
5. Biology Form Five by TIE
6. Guide to dissection by H.G.Q Rowett (2005)

**CHEMISTRY**

1. Modern ABC Chemistry for Class XI & XII
2. Inorganic By TIE
3. Physical Chemistry by TIE
4. Organic Chemistry By TIE
5. General Chemistry By TIE
6. Conceptual chemistry for class XII & XI by S.K Jaini(2011).

**HISTORY**

1. Advanced level history paper one & two by Zisti Kamili.
2. Understanding African history. Advanced level paper one by Joannes Biginuamungu
3. Mastering advanced level history book One & Two (2010) by Kato, A.
4. Contemporary history events. paper 1 &2 BY Shibitali C.K
5. History from 5&6 by Scsu & MoEVT-Zanzibar
6. History Form Five By TIE

**ENGLISH LANGUAGE**

1. Advanced literature by Nyambari Nyangwine
2. The real English Advanced level by Dr. Michael Kadeghe.
3. New advanced level English by Charles E. Shalua
4. Introduction of phonology by Gimson
5. A University grammar of English
6. A complete English course for form V & VI by Dr. Michael Kadeghe
7. Oxford advanced learners dictionary

**GEOGRAPHY**

1. Physical Geography by TIE
2. Practical geography by TIE
3. Human Economic Geography by TIE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MARA
S.L.P 193, MUSOMA Email: marasec123@gmail.com
Tovuti: www.marasecondaryschool.blogspot.Com

**MEDICAL FORM NO 1**

To be Completed by a Medical officer in respect of all one(s) new entrants

Full Name: ..........................................................................................................

Age............................................... Year .....................................Sex.......................

Blood count (Red and white).................................................................................

Stool examination....................................................................................................

Urine analysis...........................................................................................................

Syphilis Test. ............................................................................................... T.B

Test..........................................................................................................

Ears.........................................................................................................

Chest.......................................................................................................

Spleen....................................................................................................

ADDITIONAL INFORMATION e.g Physical detects or impairment Infections, Chronic of family diseases etc.

......................................................................................................................

......................................................................................................................

......................................................................................................................

From the results shown above. I certify that the above student is fit/unfit to pursue studies.

Signature...............................................................................................

Designation............................................................................................

Station.....................................................................................................